HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA

Simu:
Mkurugenzi wa Jiji: 27 2643068
Idara zote: 27 2644530/3
Fax: 255 27 2644141/27 2647905
E-Mail: info@tangacc.go.tz

Barabara ya Hassani Ngwilizi
S. L. P. 178,
Tanga.

Tanzania.

03/05/2019

TANGAZO

TANGAZO LA ZABUNI YA UWAKALA WA UKUSANYAJI WA USHURU WA MAPATO HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA

1. Halmashauri ya Jiji la Tanga inawatangazia wafanyabiashara/makampuni/ushirika/vikundi kuwa inahitaji kupata wazabuni wenye uwezo wa kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri kuanzia tarehe 01/07/2019 Hadi 30/06/2020 kwa mujibu wa sheria ndogondogo za Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali hapo chini:-
2. Zabuni zinazotangazwa ni **LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01**

LOT YA NUKUU YA BEI	JINA LA ZABUNI
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 1	Ushuru wa choo cha soko la Makorora
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 2	Ushuru wa choo cha soko la Mlango wa chuma
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 3	Ushuru wa choo cha soko la kisosora
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 4	Ushuru wa choo cha soko la Ngamiani
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 5	Ushuru wa choo cha Msambweni (Bus stand ya Pangani)
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 6	Ushuru wa choo cha soko la Mkwakwani
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 7	Ushuru wa choo cha bustani ya sakarani
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 8	Ushuru wa vyoo vya soko la Mgandini
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 9	Ushuru wa choo cha soko la Majengo
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 10	Ushuru wa choo cha gulio la Tangamano
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 11	Ushuru wa choo cha Bus stand mpya (Kange)
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 12	Ushuru wa choo cha Bus stand ya zamani (Ngamiani)
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 13	Ushuru wa mizigo katika soko la Mgandini na Mlango wa chuma.
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 14	Ushuru wa Mkaa, kuni na Mirunda.
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 15	Ushuru wa Samaki vituo vya kukusanyia samaki Kasera na Mchukuuni
LGA/128/2019-2020/NC/HQ/01 Lot 16	Ushuru wa Samaki vituo vya kukusanyia samaki Deep sea

Masharti kwa waombaji

i. Muombaji asiwe anadaiwa Halmashauri kwa namna yoyote.

ii. Ada ya maombi ya zabuni ni Tshs. 50,000/= ambazo hazitarejeshwa, zilipwe fedha taslim na atapewa seti ya Kabrasha la zabuni.

iii. Nakala ya stakabadhi itaambatanishwa kwenye kabrasha la maombi ya zabuni.

iv. Ada ya maombi uliyolipa ni kwa ajili ya kupata maelekezo ya zabuni (Kabrasha la zabuni), katika kabrasha la zabuni hiyo kuna masharti na vigezo vya nyongeza kwa zabuni hii. Maelekezo ya zabuni yanapatikana kwa katibu wa bodi ya zabuni.

v. Muombaji awe na Leseni hai ya biashara, inayohusiana na kazi anayoomba.

vi. Muombaji atakayeshinda zabuni atatakiwa kuweka Deposit (Dhamana) ya miezi mitatu kwa kiasi alichoomba kabla hajasaini mkataba.

vii. Mwombaji aeleze eneo la biashara au kampuni ilipo **(Physical location)**

viii. Muombaji lazima ahakikishe eneo la kazi linakuwa safi muda wote

ix. Mkataba utakuwa wa miezi 12 kuanzia tarehe 1 July 2019 hadi tarehe 30 June 2020.

x. Wakala atatakiwa kuwasilisha fedha yote aliyokusanya kila siku na endapo atashindwa kutekeleza sharti hilo atakuwa amevunja masharti ya Mkataba.

xi. Mwombaji aonyeshe asilimia ngapi anayotarajia kurejeshewa na Halmashauri baada ya Kuzingatia kipengele **No X** cha masharti ya Zabuni hii.

xii. Muombaji lazima aonyeshe uthibitisho wa kulipa kodi (Tax clearance certificate) kutoka TRA.

xiii. Muombaji hatakiwi kuwa mtumishi au kiongozi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga

xiv. Muombaji awe na Taxpayer Identification Number (TIN)

xv. Mwombaji aambatanishe hati ya uthibitisho wa kisheria – (Power of attorney) ya mtu anayehusika na zabuni hii.

xvi. Mwombaji atoe mchanganuo wa mapato na matumizi wa Jinsi atakavyokusanya ushuru wa chanzo anachoomba.

xvii. Muombaji ataje makadirio ya makusanyo atakayowasilisha Halmashauri kwa mwezi.

xviii. Mzabuni atakayeshinda atalazimika kukusanya ushuru na kutoa risiti kwa kutumia mashine za POS atakazopewa na Halmashauri.

xix. Mzabuni atakayeshinda atawajibika kutunza POS, uharibifu wowote utakaotokea atawajibika kugharamia.

xx. Mzabuni atakayeshinda atawajibika na uharibifu wowote atakaosababisha na kuathiri ukusanyaji wa mapato.

xxi. Asiwe mtengeneza migogoro na Halmashauri

xxii. Asiombe zabuni na kuingia makubaliano ya ukusanyaji na mtu mwingine.

xxiii. Asiwe msumbufu wa kulipa kodi za Serikali.

xxiv. Mwombaji kabla ya kuomba zabuni, afanye utafiti wa kina kwa chanzo anachotarajia kuomba.

Kwa wafanyabiashara/Makampuni/Vikundi/Ushirika ambao watapenda kutoa huduma eneo mojawapo kati ya yalizoorodheshwa hapo juu, wafike katika ofisi ya **KATIBU WA BODI YA ZABUNI** ya Halmashauri ya Jiji la Tanga iliyopo barabara ya Hassani Ngwilizi S.L.P. 178 Tanga chumba namba 6 kupata:

. Maelezo zaidi yanayohusiana na zabuni hizi

. Kununua Kabrasha la zabuni ambalo linauzwa Tshs.50,000/= fedha ambazo hazitarudishwa.

. Kupata nyongeza (Addition/Ammendment) ya kabrasha la zabuni kama zitakuwepo.

JINSI YA KURUDISHA ZABUNI

Mzabuni atatakiwa kujaza bei, na kutoa maelezo kwa ufasaha kulingana na maelezo yaliyopo katika kabrasha la Zabuni.

Kabrasha la zabuni baada ya kujazwa kama ilivyoelezwa hapo juu itolewe nakala moja, zote mbili kwa pamoja zifungwe kwenye bahasha na kuwekwa lakiri(seal) juu ya bahasha isionyeshe alama yeyote ile mbali na tulivyoelekeza. Juu ya bahasha iandikwe jina la zabuni na namba ya zabuni unayoomba na itumwe kwa;

KATIBU WA BODI YA ZABUNI
S.L.P. 178
TANGA

Zabuni zinaweza kupelekwa kwa Mkurugenzi kwa kutumia Posta au kwa mkono siku ya mwisho kupokea zabuni ni siku ya **Jumatatu ya tarehe 20/05/2019 Saa 4:00 asubuhi** na ufunguzi utafanyika siku hiyo hiyo muda mfupi tu baada ya zabuni kupokelewa mbele ya wazabuni au wawakilishi wao watakaopenda kuhudhuria.

MKURUGENZI WA JIJI
TANGA